# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

---

**UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote naomba kuanza hotuba hii, kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia afya njema na kuweza kukutana hapa katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Baraza la Kumi la Wawakilishi kwa lengo la kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa kutimiza azma ya Serikali yetu ya kuwapelekea wananchi maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuongoza, kutuelekeza na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mujibu wa Katiba na kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025, MKUZA III na Mipango mikuu ya Maendeleo kwa Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kumpa afya njema, hekma na busara katika kulingoza taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Abdulla Suleiman kwa kutekeleza vyema majukumu yake ya kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Ofisi hii lakini pia kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kupitia taasisi zote za Serikali

na zisizo za Serikali kwa lengo la kuimarisha uchumi wa nchi na kukuza demokrasia nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kukushukuru wewe binafsi kuweza kunipatia nafasi hii mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na muelekeo wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 ambayo lengo lake kuu ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali katika sekta zote za SMZ na masuala ya Muungano kwa kufuata misingi ya Katiba na Sheria pamoja na kufuata misingi ya haki za binaadamu na ushirikishwaji.

**Mheshimiwa Spika,** Nitumie pia fursa hii, kuipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na kumpongeza yeye binafsi kwa kusimamia na kuongoza vyema majukumu yake kwa mashirikiano na watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wake, Dkt. Islam Seif Salum kwa utendaji mzuri wa kazi zao na ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake. Sambamba na hayo, niishukuru Ofisi hii kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu bajeti yao kwa mwaka 2023/2024 kwa wakati, huku ikiainisha vipaumbele vyote ambavyo msingi wake ni kuleta maendeleo chanya kwa wazanzibari.

**Mheshimiwa Spika**, Vile vile, pongezi za dhati kabisa ziende kwa wajumbe wa Kamati yangu kwa kazi nzuri wanayoifanya na ushirikiano wanaouonesha kwa pamoja katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu kwa muda wote, naomba sasa niwatambue wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said — Mwenyekiti
2. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Suleiman Makame Ali — Mjumbe
4. Mhe. Zaina Abdalla Salum — Mjumbe
5. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha — Mjumbe
6. Mhe. Salma Mussa Bilal — Mjumbe

Aidha, Kamati hii inaratibiwa kazi zake na Makatibu wawili pamoja na Mkalimani mmoja wa lugha za alama ambao wanatusaidia kutekeleza majukumu yetu kitaalamu na kiufanisi, Makatibu hao ni:-

1. Ndg. Ali Alawy Ali - Katibu
2. Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir - Katibu, na
3. Ndg. Amina Abeid Hemed - Mkalimani.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi yenye mafungu matatu (03) ambayo ni Fungu C01 Ofisi Kuu, fungu C02 Baraza la Wawakilishi na fungu C03 Tume ya Uchaguzi, Mafungu haya yanaendeshwa kwa Progaramu Kuu 07 na Programu Ndogo 14 ambazo zimo katika kila fungu husika kama zilivyoainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kitabu cha Bajeti kuu.

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Program hizi umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, Mpango wa kukuza uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2025, Ahadi zinazotolewa na Mhe Rais Dkt Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika ziara zake mbali mbali, pamoja na Hutuba na maagizo ya Mheshimiwa Rais ambayo anayatoa kila anapopata fursa ya kufanya hivyo kwa ajili ya kujenga mustakbali uliobora wa maendeleo ya nchi yetu.

**FUNGU C01: AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

**Mheshimiwa Spika**, Katika fungu C01; Kupitia program kuu ya ***Uratibu wa Shughuli za Serikali:*** Kamati inaipongeza Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi viongozi wa kitaifa kwa kusimamia vyema malengo yake na kuhakiksha yanaenda kama yanavyopangwa. Aidha, Kamati inashauri kuongeza juhudi katika kuboresha shughuli zake kwa kuimarisha vifaa vya ukodishaji na

kuhakikisha wanaenda sambamba na mabadiliko ya kimaendeleo. Kamati pia, inashauri Idara ya Sherehe kununua vifaa vipya na vya kisasa ambavyo vitaweza kuwaingizia mapato pamoja na kutumika katika sherehe mbali mbali za kitaifa na kijamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyofahamu kuwa suala la maafa katika jamii haliwezi kuepukika kwa kutumia tu juhudi za wanaadamu bali ni matukio ya kimaumbile katika kutokea kwake; lakini tunaweza kukabiliana nayo wakati yanapotokea ili kupunguza athari za moja kwa moja kwa jamii. Kupitia program ndogo ya SC010201 **Kukabiliana na Maafa**: Kamati yangu inashauri Idara ya Kukabiliana na Maafa kushirikishwa moja kwa moja katika kazi za mipango miji ambazo zinafanywa kila siku kwani maafa zaidi yanayotokea katika nchi yetu husababishwa na miundombinu mibovu ambayo imetokana na ujenzi holela wa makaazi ya watu pamoja na barabara zisizofuata utaratibu unaofaa katika ujenzi wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia Programu ndogo ya **Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar** ambayo ina jukumu la kuratibu shughuli za SMZ, mambo ya Muungano, utafiti wa kitaifa pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) hapa Zanzibar. Katika kupunguza hali ya umasikini Vijijini kupitia Mradi wa TASAF III kwa upande wa Zanzibar, Kamati inazipongeza Serikali zetu zote mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendesha mradi huu ambao unasaidia sana wananchi wetu kujikwamua na hali ngumu ya umasikini.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, kupitia programu hii Kamati inashauri zoezi la usajili wa wananchi katika mradi huu kuzingatia sifa na vigezo vya mradi kwa maeneo yote ya vijijini ili kuepusha malamiko na matumizi mabaya ya fedha bila kufikiwa malengo. Ni imani ya Kamati yangu kwamba fedha zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha zitafikia malengo ya TASAF III na wananchi wataweza kunufaika kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa Mradi huu unafanyakazi kwa kuwafikia walengwa na kuwanufaisha, Kamati yangu inatoa pongezi

kwa uongozi wa TASAF kwa kuwapatia wajumbe wa Kamati fursa ya kutembelea baadhi Mikoa ya Tanzania Bara na kujionea jinsi wenzetu wanavyonufaika kupitia mradi huu kwa kukutana na wanufaika wenyewe na kutoa ushuhuda juu ya jinsi mradi ulivyowainua kutoka hali ngumu ya umasikini na kuwa katika hali ya kujikimu. Kwa mara nyengine tena Kamati yetu inapenda kushauri Serikali kuchukua juhudi zaidi ili Zanzibar iweze kupata miradi mikubwa ya OPEC kupitia TASAF ambayo itayosaidia kujikwamua zaidi kiuchumi.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha Ofisi ndogo ya Serikali iliyopo Dodoma kupitia Programu Ndogo ya SC010204 ambayo imepangiwa malengo kadhaa yenye mnasaba na juhudi za kuimarisha huduma kwa taasisi za SMZ Tanzania Bara. Kamati yangu inathamini mchango wake kupitia watendaji wa Ofisi hii kwa lengo la kuimarisha mawasiliano ya Serikali baina ya Taasisi za Zanzibar na zile za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, washirika wa Maendeleo na asasi za kiraia na kimataiafa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaiomba Serikali kuzidisha kasi ya kuimarisha ofisi ya Dodoma kama kiungo muhimu katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kuyadhibiti maeneo iliyopatiwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za viongozi wakuu wa Zanzibar na kuhakikisha mpango wa ujenzi wa maeneo hayo umepangwa na kutekelezwa kabla ya maeneo hayo kuvamiwa kwa shughuli nyengine za kitaifa.

**Mheshmiwa Spika,** Sote ni mashuhuda juu ya umuhimu wa Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo kwa Waheshimiwa Wawakilishi katika kuleta maendeleo ya majimbo yao, Kamati inaishauri Ofisi ya makamo wa Pili wa Rais, kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo ambayo tayari imeshapata maoni kutoka Tume ya kurekebisha Sheria. Kamati inaiomba Ofisi wakati wa marekebisho ya Sheria hiyo kuzingatia zaidi mgao wa fedha za Mfuko huo zinazotolewa kwa Wajumbe kwa kuzingatia ukubwa wa Jimbo, Idadi ya watu kwa mujibu wa Sensa ya 2022 na hali za wananchi wa Jimbo husika.

**FUNGU C02: AFISI YA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Baraza la Wawakilishi yenye fungu C02, kupitia programu ndogo ya SC020201 **Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi,** Kamati imefarajika sana kuona jinsi mipango na mashauri mbali mbali yanavyo tekelezwa siku hadi siku na hivyo kupelekea kuimarika kwa dira na malengo ya Baraza hapa Zanzibar na nje ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati imeshauri wataalamu wa usanifu majengo wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kushirikiana na Wataalamu wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa lengo la kuandaa mchoro ambao utatumika kwa upanuzi wa jengo la ofisi ili kutatua changamoto ya nafasi kwa watendaji wa kada mbali mbali. Sambamba na hayo, Kamati pia inaishauri Afisi ya Baraza kupitia kitengo cha Utafiti kutafuta wafadhili ambao watasaidia kufadhili program za mafunzo kwa wajumbe na watendaji ili kuwajengea uwezo wa kiutendaji.

**FUNGU C03: TUME YA UCHAGUZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa kazi zake nzuri na zenye manufaa kwa wananchi na mustakbali wa kukuza demokrasia Zanzibar. Hata hivyo, Tume ya Uchaguzi Zanzibar inakabiliwa na changamoto ya majengo ya ofisi za Wilaya na vyombo vya usafiri kwa Unguja na Pemba na hivyo kulazimika kuazima magari kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali na majengo ya ofisi ili kupata kutekeleza majukumu yake kiufanisi. Kamati inashauri, Serikali kuandaa mpango maalumu wa kujenga ofisi za wilaya kwa Mikoa yote ya Unguja na Pemba ili kuifanya Tume ya Uchaguzi kuwa na mawanda mapana zaidi katika kutekeleza majukumu yake.

**HITIMISHO:**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaiomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhakikisha wanasimamia vyema ukusanyaji wa mapato kupitia vianzio vyao vilivyopo ili kuweza kuongeza ufanisi katika kazi zao na mapato kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kupitia Bajeti hii ya 2023/2024 Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati ili Taasisi zilizochini ya Ofisi hii ziweze kutekeleza majukumu yake kwa weledi na kukamilisha malengo yao kwa maendeleo ya wananchi na Nchi kwa ujumla, Kwani, kucheleweshwa kwa fedha za matumizi mengineyo kunapelekea watumishi kutolipwa stahiki zao mbali mbali kwa wakati ilhali ni haki zao kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, ili kufikiwa malengo waliyojipangia katika utekelezaji wa majukumu yao, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi na kwa niaba ya Kamati hii tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie na wairidhie Bajeti hii na hatimae wapitishiwe makadirio ya mapato na matumizi ya fedha zilizopangwa kwa ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**

*Kwa niaba ya Kamati yangu* ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

……………………………

**(Machano Othman Said)**
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA**
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR.**